

#MAKINIKIA Kutoka Kitabu Becoming Supernatural (Ijue Nguvu Kubwa Ya Kufanya Miujiza Iliyopo Ndani Yako Na Jinsi Ya Kuitumia Kufanikiwa)

Rafiki yangu mpendwa,

Karibu kwenye mafunzo ya ziada (#MAKINIKIA) kutoka kwenye kitabu kinachoitwa Becoming Supernatural: How Common People Are Doing the Uncommon kilichoandikwa na Dr. Joe Dispenza.

Kupitia kitabu hiki tumejifunza nguvu kubwa ya kufanya miujiza ambayo ipo ndani ya kila mmoja wetu. Tumeona vikwazo vya nguvu hii na jinsi ya kuvivuka ili kuweza kufanya miujiza kwenye maisha yetu.

Kama ambavyo tumejifunza, msingi mkuu wa sisi kuweza kufanya miujiza unaanzia kwenye kutuliza akili yetu, kuiondoa kwenye hali ya msongo na kuweza kuunganisha akili na moyo katika kuzalisha mawimbi yanayotuganisha na mawimbi yanayoendesha dunia, ambayo ndiyo chanzo kikuu cha miujiza.

Njia pekee ya sisi kuweza kushika udhibiti wa akili zetu ni kupitia tahajudi. Katika kitabu hiki, mwandishi ametushirikisha tahajudi mbalimbali za kufanya ili kuweza kuiweka akili na miili yetu katika hali ya kupokea miujiza mikubwa.

Katika mafunzo haya ya ziada, nakwenda kukushirikisha TAHAJUDI TANO za kufanya na jinsi ya kuzifanya ili uweze kutengeneza miujiza kwenye maisha yako.

Karibu ujifunze, uweze kuchukua hatua ili kutengeneza miujiza mikubwa.

MOJA; TAHAJUDI YA KUINGIA KWENYE UWEZO MKUBWA WA ULIMWENGU.

Tahajudi ya kuingia kwenye uwezo mkubwa wa dunia ni tahajudi ya kukuunganisha wewe na mawimbi makubwa anayoendesha dunia. Kama tulivyojifunza, miujiza inatokea pale mawimbi ya akili na mwili wako yanapoendana na mawimbi yanayoiendesha dunia.

Katika kufanya tahajudi ya kuingia kwenye uwezo mkubwa wa ulimwengu, fanya yafuatayo;

1. Kufanya tahajudi hii chagua chumba chenye utulivu, ambapo unaweza kukaa chini na kufunga macho ili kufanya tahajudi.
2. Weka umakini wako kwenye kila eneo la mwili wako na nafasi zinazozunguka eneo hilo. Anzia chini ya mwili na panda kuelekea kichwani. Kila unapoweka umakini kwenye eneo, nguvu zako zinaenda pale.
3. Tambua uwazi uliopo kati yako na dunia, angalia utupu ulipo kwenye chumba unachofanyia tahajudi. Huu ni wakati wa kuondoa umakini wako kwenye mwili wako na hata kwako binafsi na kuuweka kwenye utupu unaokuzunguka na kuizunguka dunia. Utupu huu siyo kwamba hauna kitu, bali una mawimbi yanayoiendesha dunia.
4. Fikiria uwezo mkubwa uliopo kwenye utupu unaoonekana kwenye dunia. Fikiria mawili yote ya redio, simu na mawasiliano mengine yanapita kwenye utupu huo. Kwa kufikiria hivi, unaunganisha mawimbi yaliyo ndani yako na mawimbi haya yanayoendesha dunia, na unajiona kuwa kitu kimoja na mawimbi hayo.
5. Unapofika katika hatua hii ya kujiona kwenye umoja na mawimbi yanayoendesha dunia, jiachilie kwenye mawimbi hayo, ukiamini nguvu yake ni kubwa na itakuwa na manufaa kwako. Usiogope kujiachilia kwenye nguvu hii kwa kung'ang'ana na yale uliyonayo, kubali kutokuwa yeyote ili kufaidi nguvu hii kubwa. Ukiwa katika hali hii bariki mwili wako na maisha yako yote, nguvu hii kubwa italeta matokeo ya tofauti kwenye maisha yako.
6. Maliza tahajudi hii kwa kurudisha umakini wako kwenye chumba ulichopo, fungua macho yako na ondoka kwenye tahajudi hii kama tayari umeshapokea kile ambacho unataka kupata.

MBILI; TAHAJUDI YA KUBARIKI VITUO VYA NGUVU.

Kama tulivyojifunza, tuna vituo nane vya nguvu, saba vipo ndani ya mwili, kimoja kipo nje ya mwili. Katika tahajudi hii, tunakwenda kuvibariki vituo vyote vya nguvu, ili tuweze kutumia nguvu za vituo hivi katika kutenda miujiza.

Katika kufanya tahajudi hii, zingatia yafuatayo;

1. Anza kwa kuweka umakini wako kwenye kituo cha kwanza cha nguvu kisha peleka umakini wako kwenye eneo linalozunguka kituo hicho cha kwanza.
2. Baada ya kuweka umakini kwenye eneo linalozunguka kituo hiki cha kwanza, bariki eneo hilo kwa kulitakia mema na kuunganisha na hisia chanya kama upendo, shukrani na furaha. Hisia hizi zinakuza mawimbi ya kituo hiki.
3. Fanya hivi kwa kila kituo mpaka kufika kitu cha saba. Unapofika kitu cha nane, ambacho kipo inchi 16 juu ya kichwa, bariki eneo hili kwa shukrani na kuthamini. Kituo hiki ndiyo kinachofungua mlango wa wewe kuingia kwenye mawimbi yanayoendesha dunia.
4. Ukiwa kwenye kituo cha nane, weka umakini wako kwenye mawimbi yanayozunguka mwili wako. Kwa kufanya hivi unapata nguvu zaidi kutoka kwenye mawimbi hayo, nguvu zinazokuwezesha kukuza zaidi mawimbi ya mwili wako.
5. Ili kupata kile unachotaka kwenye tahajudi hii, lazima kwanza uwe na hisia za kuwa na kitu hicho. Kama unataka kupokea uponyaji lazima ujione ukiwa mkamilifu.
6. Baada ya kumaliza kubariki vituo vyote vya nguvu, jilaze chini kwa dakika 15, achilia na ruhusu akili yako ya ndani ichukue nafasi ya kuipokea nguvu ya mawimbi uliyojiunga nayo.

TATU; TAHAJUDI YA KUFUNGUA AKILI YA MOYO.

Hii ni tahajudi ya kuweza kutumia nguvu kubwa ya moyo wako katika kuleta miujiza. Kama tulivyojifunza, miujiza hutokea pale moyo na akili vinapofanya kazi kwa pamoja.

Hatua za kufanya kwenye tahajudi ya kufungua akili ya moyo;

1. Funga macho yako na ruhusu mwili wako ulegee na weka umakini wako kwenye moyo wako. Anza kupumua kwa kina na taratibu, huku fikra zako zote zikiwa kwenye eneo la kifua.
2. Ukiwa bado umakini wako uko kwenye kifua, huku ukipumua, ibua hisia chanya ndani yako, zisikie hisia hizi zikiwa kwenye moyo wako. Tuma nguvu hii kubwa ya hisia kwenda nje ya mwili wako na unganisha nguvu hii ya hisia na nia uliyonayo kwenye kile unachotaka.
3. Endelea kutuma nguvu zako za hisia na nia ya unachotaka kwa dakika kumi na rudia hivi kila siku.

4. Tahajudi hii inafanya kazi ya kuunganisha moyo wako na akili yako, vitu hivi vinapofanya kazi pamoja, unakuwa na nguvu kubwa ya kutenda miujiza.

NNE; TAHAJUDI YA KUTEMBEA.

Hii ni tahajudi unayoifanya ukiwa umesimama au ukiwa unatembea. Ni tahajudi yenye nguvu kwa sababu unauweka mwili kwenye mwendo wa kuiendea miujiza yako.

Hatua za kufanya tahajudi hii;

1. Tafuta eneo tulivu kwenye mazingira ya asili. Jitenge na mazingira ya nje, funga macho na peleka umakini wako kwenye eneo la moyo. Ibua hisia chanya ndani yako, kama shukrani, upendo, huruma.
2. Ukiwa bado umeweka umakini wako kwenye kifua, endelea kupumua kwa kina na taratibu huku ukiulegeza mwili wako kwa dakika mbili, kisha rudi kwenye kuibua hisia chanya kwa dakika tatu. Tuma nguvu zinazojengeka ndani yako kwenda kwenye mazingira yanayokuzunguka.
3. Weka picha ya kile unachotaka kwenye akili yako, na jiweke kwenye hisia kama tayari umeshakuwa nacho. Endelea kutuma nguvu na mawimbi kwenye mazingira yanayokuzunguka, shikilia picha hiyo kwa dakika tatu.
4. Fungua macho yako na anza kutembea bila ya kuangalia pembeni au kumwangalia yeyote. Unapotembea, endelea kutoa mawimbi na nguvu na jione ukitembea kuelekea kwenye kesho yako iliyo bora, ukiwa na hisia kama tayari umeshapata unachotaka.
5. Jikumbushe picha ya kile unachotaka, na jione kama tayari umeshakipata, furahia kukipata na kuwa sehemu ya kitu hicho. Tahajudi hii ina nguvu kubwa ya kukupeleka kwenye yale maisha unayoyataka.

TANO; TAHAJUDI YA KUCHOCHEA TEZI YA PINEA.

Tezi ya pinea ndiyo tezi kuu ya miujiza kwenye akili yetu. Ni kituo cha sita cha nguvu. Tezi hii huzalisha homoni ya melatonin ambayo ina mazao yake yenye nguvu kubwa ya kuleta mabadiliko ya kiakili.

Kwa kuamsha na kuchochea tezi hii kuzalisha homoni ya melatonin na kuweka nguvu kubwa kwenye tezi hii, inatuunganisha na nguvu kubwa ya mawimbi inayoongeza dunia na kuweza kutenda miujiza mikubwa.

Hatua za kufanya tahajudi ya kuchochea tezi ya pinea;

1. Anza kwa tahajudi ya kubariki vituo vya nguvu, kuanzia kituo cha kwanza mpaka kufika kituo cha sita. Kwa kufanya tahajudi hii, unakusanya nguvu kutoka vituo vya chini na kuiweka kwenye kituo cha sita, nguvu hii inachochea uzalishwaji wa melatonin.
2. Baada ya nguvu kufika kwenye kituo cha sita, ipeleke kitu cha saba na cha nane wakati huo unapumua kwa kina, kitu ambacho kinachochea pinea kuzalisha zaidi melatonin.
3. Kwa nguvu kubwa inayozalishwa na homoni inayozalishwa, pamoja na kuunganika na kituo cha nane, funguka na pokea nguvu kubwa ya mawimbi yanayoendesha dunia. Kadiri unavyofunguka na kupokea nguvu hii ndivyo mawimbi ya mwili wako yanakuwa juu na nguvu inakuwa juu pia na hii inazalisha melatonin zaidi. Hivyo unakuwa ni mzunguko unaojirudia, na mzunguko huu ndiyo unaopelekea miujiza mikubwa kutoka.
4. Ukiwa unafanya tahajudi hii ya kuchochea pinea, usiweke mategemeo yoyote, wewe jiachilie kwenye huo mzunguko na nguvu kubwa inayozalishwa itakuwezesha kufikia nguvu ya juu kabisa ya mawimbi yanayoendesha dunia na hapo ndipo miujiza mikubwa inapotokea.

Rafiki, hizi ndizo tahajudi tano muhimu unazopaswa kuzifanya ili kuweza kutumia uwezo wako mkubwa kutengeneza miujiza kwenye maisha yako.

Unaweza usielewe tahajudi hizi kwa kusoma mara moja, hivyo rudia kusoma makala ya uchambuzi wa kitabu, kisha rejea kusoma tena tahajudi hizi na anza kujaribu moja baada ya nyingine.

Kadiri unavyoendelea kufanya tahajudi hizi, ndivyo utakavyogundua nguvu kubwa iliyopo ndani yako na kuweza kuitumia. Kwa kusoma pekee unaweza kuona kama ni mambo ya kusadikika, lakini unapotuliza akili yako na kufanya, unaanza kuona nguvu ambayo unayo muda wote lakini umekuwa huitumii.

Nakutakia kila la kheri katika kutumia uwezo mkubwa uliopo ndani yako kufanya miujiza mikubwa kwenye maisha yako.

Uchambuzi huu wa kitabu umeandaliwa na Dr. Makirita Amani.

Dr Makirita ni daktari wa binadamu, kocha wa mafanikio, mwandishi na mjasiriamali. Kuendelea kupata chambuzi hizi za vitabu kwenye TANO ZA JUMA, hakikisha unajiunga na channel ya TANO ZA JUMA ambayo ipo kwenye mtandao wa telegram.

Kujiunga ni bure kwa juma la kwanza, kisha baada ya hapo unachagua kulipa tsh elfu moja kwa juma, au elfu tatu kwa mwezi au elfu 30 kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi tuma ujumbe kwenda namba 0717396253, ujumbe utumwe kwa njia ya telegram pekee.

Karibu sana.